# HALMASHAURI YA WILAYA UVINZA

**KIZIDUO CHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA UGAWAJI ARDHI KILICHOFANYIKA TAREHE 25/10/2018 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Arch. Weja L. Ng'olo | -Mkurugenzi Mtendaji | -Mwenyekiti |
| 2. Ndg. Paul A. Misuzi | –Afisa Ardhi Mteule | -Katibu |
| 3. Ndg. Makongo Manyama | -Afisa Ardhi | -Mjumbe |
| 4. Mhe. Salome L. Luhinguranya | -Diwani V/Maalum Ilagal | -Mjumbe |
| 5. Mhe. Kafunya K. Kafunya | -Diwani Kata Ilagala | -Mjumbe |
| 6. Ndg. William Maswi | -Afisa Mipango miji | -Mjumbe |
| 7. Ndg. Msongo Songoro | -Afisa Mifugo na Uvuvi | -Mjumbe –Mwalikwa |

**AJUMBE WASIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Ndg. Daniel Kamwela | -Afisa Kilimo na Umwagiliaji | -Mjunbe | -Amehama |
| 2. Ndg. Majaliwa Andrea | -Afisa Mifugo na Uvuvi | -mjumbe | -Amehama |

**SEKRETARIETI**

1. Ndg. Charles S. Robert -Mwandishi wa Vikao

**AGENDA NA. 01: MUHT. NA. 01/2018/2019 KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao. Mwenyekiti akifungua kikao aliwakaribisha wajumbe na kuwataarifu kuwa kama tutafanikiwa jambo la kukodisha mashamba ni chanzo kikubwa cha mapato kwa Halmashauri pia suala la wajumbe waliokuwa wameteuliwa baada ya kugundua utaratibu umekiukwa tuliona muendelee na kwamba katibu wa kikao hayupo lakini ameruhusu kikao kiendelee kisha alifungua kikao mnamo saa 5.20 asubuhi

**AGENDA NA. 02: MUHT. NA. 02/2018/2019 KUTHIBITISHA AGENDA**

Agenda zilisomwa na kuthiibitishwa na wote kama ifuatavyo:-



Certified True copy of the original document
DLO

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha Agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 25/10/2018
4. Kuwasilisha taarifa ya ugawaji mashamba yaliyopimwa
5. Kuidhinisha ugawaji wa eneo lenye ukubwa wa ekari 207 katika Kijiji cha Rukoma
6. Kupitisha maombi ya kumiliki ardhi katika ardhi ya jumla eneo la Ngogomyi
7. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
8. Kufunga kikao

**AGENDA NA. 05: MUHT. NA. 05/2018/2019 TAARIFA YA UGAWAJI WA ENEO LENYE UKUBWA WA EKARI 207 KATIKA KIJIJI CHA RUKOMA**

Taarifa ya kuidhinisha ugawaji wa eneo lenye ukumbwa wa ekari 207 katika Kijiji cha Rukoma ili kutumika kwa ajili ya uwekezaji wa mradi wa kufua umeme toka maporomoko ya maji mto Luegere, iliwasilishwa na kupokelewa na wajumbe pia walifanya mjadala kama ifuatavyo:- Wajumbe walihitaji kujua kusudi la mradi huo na kama taratibu zimefuatwa kwa kampuni hiyo ya ARMSTONE kupewa kiasi hicho cha Ardhi kwa kuwa uwezo wa Kijiji kutoa eneo mwisho ni ekari 50.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa kampuni ya ARMSTONE ni kampuni ya kigeni kwa kuwa wanahisa wake wengi ni wageni. Kwa sababu hiyo eneo hilo halitamilikiwa moja kwa moja na kampuni hiyo bali litamilikiwa na kituo cha uwekezaji Tanzania (TIC) na baadae Kituo hiki kitatoa haki miliki isiyo ya asili (Derivative Right) kwa kampuni hii ya kigeni. Katika hatua, kipande hiki cha Ardhi chenye ukubwa wa ekari 207 kitatakiwa kuhamishwa usimamizi toka kuwa Ardhi ya kijiji na kuwa Ardhi ya jumla, hatua ambayo kitaalamu inaitwa Uhawilishaji na tayari kijiji wametoa na kukubali eneo hili kuhawilishwa ili litumike kwa uwekezaji wa mradi huu wa umeeme. katika kikao cha halmashauri ya kijiji na Mkutano mkuu uliofanyika tarehe 10/10/2018 ambao ulihudhuriwa na Mh. Mkuu wa wilaya kama taratibu zinavyoelekeza.

Baada ya ufafanuzi huo wajumbe walihitaji uthibitisho wa uwepo wa vielelezo mbalimbali kama mihutasari ya vikao vilivyofanyika na uhakika wa taratibu za kufuatwa ikiwa ni pamoja na uhalali wa kampuni.

Mwenyekiti aliwatoa hofu wajumbe kuwa suala hili lipo na anataarifa za hatua zote zilizofanyika ni pamoja na Mh. Mkuu wa wilaya kuhudhuria mikutano iliyotajwa na pia amekuwa akikutana mara kwa mara na mwakilishi wa kampuni husika.

Afisa Ardhi alithibitisha taratibu zote za kisheria kufuatwa, ikiwa ni pamoja na uwepo wa mihutasari yote iliyotajwa na kuwaambia wajumbe kuwa hata ombi hili kujadiliwa katika kikao hiki ni miongoni mwa kutekeleza taratibu za kisheria zilizowekwa. Na kwa kuwa ombi hili ni la uhawilishaji litafika mpaka kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya ukubali.



Certified true copy of the original document

DLO

Baada ya mjadala wajumbe walikubaliana kuridhia ugawaji wa Ardhi hiyo pamoja na kuridhia uhawilishaji wa eneo hilo ili ombi hili liendelee katika ngazi zinazofuata.

**AGENDA NA.08: MUHT.NA 07/2018/2019 KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufunga kikao. Mwenyekiti alifunga kikao na kuwashukuru wajumbe kwa kuchangia vizuri na kumaliza kikao salama kisha alifunga kikao 9:00 alasiri.

**UMETHIBITISHWA NA**

............................ ............................

KATIBU MWENYEKITI

12/11/2018
...............................

TAREHE

MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA NYINZA

Certified true copy of the original document

DLO
14/11/2019